Mwanza Urban Water Supply And Sanitation Authority

# MWAUWASA

NEWS BULLETIN

**TOLEO NAMBA: 05** OKTOBA, 2019 www.mwauwasa.go.tz

## TUNATEKELEZA KWA VITENDO



**ZIARA YA WAZIRI MBARAWA KWENYE MRADI WA MAJI MSALALA**

uk 8



**PONGEZI KWA MHANDISI ANTHONY SANGA**

uk 4

## SERIKALI YA DKT. MAGUFULI NI YA VITENDO- PROF MKUMBO

# MIRADI YA BILIONI 788 KUTEKELEZWA KANDA YA ZIWA VICTORIA

uk 2



# MIRADI YA BILIONI 788 KUTEKELEZWA KANDA YA ZIWA VICTORIA

Serikali inatekeleza miradi 17 ya maji yenye thamani ya Shilingi Bilioni 788 ikiwa ni hatua mojawapo ya utatuzi wa changamoto ya upatikanaji wa maji kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo aliyasema hayo Agosti, 2019 alipofanya ziara kwenye mradi wa maji wa Nyahiti, Wilaya ya Misungwi Mkoani Mwanza kwa lengo la kujionea hatua iliyofikiwa ya utekelezwaji wake.

Aliwaasa wananchi waendelee kuiamini Serikali ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwani hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Serikali yake kupitia Wizara ya Maji ya kuhakikisha huduma ya maji inafika kwenye maeneo yote yenye changamoto.

"Tunaendelea hatua kwa hatua kutatua changamoto ya maji kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara na kwa upande wa Kanda ya Ziwa tunatekeleza miradi 17 inayotumia maji kutoka Ziwa Victoria yeye thamani ya Bilioni 788," alisema Profesa Mkumbo.

Akiuzungumzia mradi wa maji wa Nyahiti, Profesa Mkumbo alisema gharama za utekelezaji wake ni Bilioni 13 na umekamilka kwa asilimia 97 na kwamba hatua iliyopo ni ya kuwaunganishia wananchi ambapo takriban wateja 2,150 wataunganishwa kwenye awamu ya kwanza.

Alisema mradi umesanifiwa kuhudumia wananchi wapatao 64,280 hadi ifikapo Mwaka 2040 waishio katika Mji Mdogo wa Misungwi na Vitongoji vyake, kikiwemo kijiji cha Nyahiti ulipo mradi.

Aliwaasa wananchi kuhakikisha wanautunza mradi huo ili uwe endelevu kwa miaka 20 ijayo kama ulivyosanifiwa hasa ikizingatiwa kwamba Serikali imetumia fedha nyingi kwenye ujenzi wake na pia fedha zitaendelea kutumika kwenye uendeshaji wake.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo (kulia) akisikiliza maelezo ya utekelezaji wa mradi wa Nyahiti kutoka kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (kushoto) wakati wa ziara yake ya kukagua hatua mradi. Katikati ni Mbunge wa Jimbo la Misungwi, Charles Kitwanga.

Profesa Mkumbo aliipongeza MWAUWASA kwa usimamizi mzuri wa mradi huo wa Misungwi na miradi mingine inayoisimamia ikiwemo mradi wa Magu, Mkoani Mwanza na Mradi wa Lamadi, Mkoani Simiyu.

Kwa upande wake aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga alibainisha kwamba kukamilika kwa mradi huo Nyahiti kutaongeza upatikanaji wa majisafi na salama katika mji mdogo wa Misungwi na vitongoji vyake kutoka asilimia 42 ya sasa hadi asilimia 100.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo akitembelea eneo la kutibu maji la mradi wa maji wa Nyahiti, Misungwi.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo akizungumza na wananchi wa Kisesa, Wilayani Magu (hawapo pichani).

# SERIKALI YA DKT. MAGUFULI NI YA VITENDO- PROF MKUMBO

Imeelezwa kuwa Serikali ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kumaliza kero ya maji kupitia miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa kote nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo aliyasema hayo Agosti, 2018 kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kisesa, Wilaya ya Magu ambapo aliwatoa hofu kuwa watapata huduma ya uhakika ya maji hivi karibuni baada ya kukamilika kwa mradi ambao unaendelea kujengwa.

Alisema Serikali inatambua changamoto ya upungufu wa maji inayowakabili wananchi wa Kisesa, Bujora na Bukandwe na hatua za kuondokana nayo zimeanza kuchukuliwa ikiwemo ya ujenzi wa tanki la lita milioni mbili hapo Kisesa ambalo litakamilika mapema 2020.

"Kero ya maji ni kubwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali za utatuzi wake si ahadi, inataka kupanua mtandao wa maji hapa Kisesa na kwingine ili kumaliza tatizo hilo lililodumu kwa miaka mingi. Sisi watendaji tunatoa majibu kwa kutekeleza," alisema Profesa Mkumbo.

Profesa Mkumbo aliwaasa wananchi waliopo kwenye maeneo yenye changamoto ya upatikanaji wa maji kuendelea kuwa na subira wakati Serikali ikiendelea kupata ufumbuzi wa kudumu kupitia miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa kote nchini.

"Ni busara wananchi tukatazama tulikotoka, tulipo na tunapokwenda. Serikali kwa kutambua kero kubwa ya maji inayowakabili wananchi imeamua kutekeleza miradi 17 ya kimkakati Kanda ya Ziwa itakayogharimu Sh. bilioni 788 ili kutatua changamoto hiyo kwa kutumia maji ya ziwa Victoria," alisema Profesa Mkumbo.



Baadhi ya wananchi wa Kisesa, Wilayani Magu wakimsikiliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo (hayupo pichani).

BODI YA UHARIRI

Mohamed Saif
Assistant Manager Public Relations MWAUWASA

Ikupa Enock
Graphic Designer

LIMETOLEWA NA:
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA).

0800110023
mwauwasatz
mwauwasa

MWAUWASA
Mwanza Urban Water Supply And Sanitation Authority
NEWS BULLETIN
Oktoba 2019



Waziri wa Maji, Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb) akikata utepe kuzindua rasmi mradi wa maji wa Kijiji cha Shilima, Kata ya Kikubiji, Wilaya ya Kwimba, Mkoani Mwanza.

# MAAGIZO YA WAZIRI MBARAWA KWA MAMLAKA ZA MAJI NCHINI

Mamlaka za maji zinazotumia bei za kukadiria (flat rates) kote nchini zimepewa miezi mitatu kuhakikisha zinawafungia dira za maji wateja wao wote ili kila mteja alipe gharama ya maji kwa kiasi alichotumia.

Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa (Mb) alitoa agizo hilo Septemba 14, 2019 alipokuwa akizindua mradi wa maji wa Kijiji cha Shilima Kata ya Kikubiji, Wilaya ya Kwimba Mkoani Mwanza.

Waziri Mbarawa alisema Serikali imetenga Bilioni moja kusaidia mamlaka za maji ambazo hukadiria matumizi ya maji wateja wake badala ya kutumia dira ya maji ili kuepuka kumbebesha mteja mzigo usiyo kuwa wake.

Waziri Mbarawa vilevile ameziagiza mamlaka za maji za mikoa kuhakikisha zinadhibiti upotevu wa maji kwani maji mengi yanapotea kabla ya kufika kwa wananchi sambamba na kuongeza mtandao wa maji ili kuwaunganisha wananchi wengi zaidi.

Akizungumzia mradi wa maji wa Shilima, Profesa Mbarawa alisema ujenzi wake ni utekelezaji wa Sera ya Maji pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inayoelekeza kuwapatia huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 85 wakazi wote waishio vijijini ifikapo mwaka 2020.

Aliongeza kuwa uzinduzi wa mradi huo ni awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Vijiji vya Shilima, Mhande na Izizimba.

Alibainisha kwamba mradi wa maji wa Shilima ulianza kutekelezwa mwaka 2013 na ulitakiwa kukamilika katika kipindi cha miezi sita. Hata hivyo, kutokana na udhaifu wa Mkandarasi aliyekuwa anautekeleza pamoja na usimamizi mbovu haukuweza kukamilika kwa wakati.

Waziri Mbarawa aliwapongeza wote walioshiriki kwenye ujenzi wa mradi kwa namna mbalimbali na kwa ushirikiano waliotoa kwa kipindi chote cha ujenzi wake hadi unakamilika kwa wakati kama alivyokuwa ameelekeza.

Aidha, aliwaasa wananchi wa Shilima kuhakikisha wanashirikiana kuulinda na kuutunza mradi kwa maslahi mapana ya sasa na ya vizazi vijavyo.

"Itakua ni jambo la aibu sana kama mtafanya uharibifu kwenye miundombinu ya mradi huu kwani mmeteseka sana kuusubiri mradi huu hivyo ni vyema mkashirikiana kuutunza huu ni mradi wenu," alisema Profesa Mbarawa.

Akizungumzia ujenzi wa mradi huo, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) ambaye alikuwa msimamizi mkuu wa ujenzi, Mhandisi Anthony Sanga alisema walizingatia agizo la Waziri Mbarawa na kwamba mradi huo ulikamilka tarehe 25 Agosti, 2019 kabla ya muda uliyokuwa umeelekezwa. Kwa upande wake Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kwimba, Mhandisi Boaz Matundalo alisema kuwa Kijiji cha Shilima kina wakazi wapatao 7,526 ambapo mradi huu wenye magati 35 una uwezo wa kuhudumia wakazi 8.750 ikiwa ni wastani wa watu 250 kwa kila gati.

Waziri Mbarawa tarehe 3 Julai, 2019 akiwa katika ziara ya kikazi Wilayani Kwimba alitoa ahadi ya kukamilisha mradi huo kwa kutumia wataalamu wa ndani kwa kuhakikisha wananchi wa Kijiji cha Shilima wanapata maji katika kipindi cha miezi miwili, yaani hadi kufikia tarehe 3 Septemba, 2019, ahadi ambayo hata hivyo ilikamilika tarehe 25 Agosti, 2019 siku tisa kabla ya tarehe ya makubaliano.





Baadhi ya wananchi waliofika kushuhudia uzinduzi wa mradi wa maji wa Shilima



Waziri wa Maji, Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb) akifungua bomba la maji la mradi wa Shilima wakati wa uzinduzi wa mradi huo Septemba 14, 2019

# PONGEZI KWA MHANDISI ANTHONY SANGA



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akimuapisha Mhandisi Anthony Sanga kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, Septemba 22, 2019. (Picha na Ikulu).**



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akiwa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Viongozi wengine wa Serikali Kuu katika picha ya pamoja na viongozi waliopishwa Ikulu jijini Dar es Salaam, Septemba 22, 2019 (Picha na Ikulu).**

MWAUWASA
Mwanza Urban Water Supply And Sanitation Authority
NEWS BULLETIN
Oktoba 2019

# KYAKA KUPATA HUDUMA YA MAJISAFI KUTOKA MTO KAGERA



Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa akizungumza kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kyaka (hawapo pichani) ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Dkt. John Magufuli.

Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa amewahakikishia wananchi wa Kyaka, Wilaya ya Misenyi Mkoani Kagera kupata huduma ya majisafi na salama kutoka Mto Kagera.

Kauli hiyo aliitoa Julai 12, 2019 wakati wa ziara yake Wilayani humo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli alilolitoa Julai 11, 2019.

Akiwa njiani akitokea Wilayani Karagwe kuelekea Wilayani Chato, Rais Magufuli alisimama katika Mji Mdogo wa Kyaka kusalimiana na wananchi na walimueleza kero ya muda mrefu ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama.

Rais Dkt. Magufuli alimuagiza Waziri Mbarawa kwa njia ya simu mbele ya wananchi hao kufika eneo hilo siku iliyofuata kuzungumza nao na kuhakikisha kero hiyo inatatuliwa.

Katika utekelezaji wa agizo hilo, Waziri Mbarawa akiwa ameongozana na Watendaji na Wataalam kutoka Mamlaka za Maji Mwanza (MWAUWASA) na Bukoba (BUWASA) alisisitiza kwamba Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dkt. John Magufuli imedhamiria kuwaondolea wananchi wake kero ya maji na aliwahakikishia wananchi wa Kyaka kwamba kero ya maji inakwenda kuwa historia.

Profesa Mbarawa alisema Mkandarasi mahiri atapewa jukumu hilo la kujenga mradi wa maji na aliwasihi wananchi hao wa Kyaka kutakapojengwa chanzo cha maji kutoa ushirikiano kwa Mkandarasi atakayetekeleza mradi ili ukamilike kwa wakati na kwa kiwango.

"Tumesema sasa imetosha wananchi kuhangaika, tunawahakikishia wananchi wote wa Kyaka kuwa mtapata majisafi na salama kutoka Mto Kagera, tunajenga mradi mkubwa wa maji ambao pia ni endelevu," alisema Waziri Mbarawa.

Waziri Mbarawa alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, wakati huo Mhandisi Anthony Sanga (sasa ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji) kushirikiana na Mkurugenzi wa Maji Bukoba, Allen Marwa na wataalam wengine kutoka Wizara ya Maji kutathmini na kuratibu haraka shughuli za ujenzi wa mradi.

Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wananchi wa maeneo ya Kyaka, Bunazi na maeneo mengine yanayozunguka mradi.



Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa (kulia) akitoa maelekezo ya utekelezaji wa mradi wa maji Kyaka kwa wataalam alipotembelea aneo linalopendekezwa kujengwa tenki la maji. Kushoto ni aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga ambaye sasa ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji.



Muonekano wa Mto Kagera kutokea eneo linalopendekezwa kujengwa tenki la maji Kyaka.



Baadhi ya wananchi wa Kyaka wakimsikiliza Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa (hayupo pichani).



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Shilima na vijiji vya jirani wakimsikiliza Mbunge wao Shanif Mansoor (hayupo pichani) wakati wa sherehe za kuupokea mradi wa maji wa Shilima.



Mbunge wa Jimbo la Kwimba Mhe. Shanif Mansoor (CCM) (katikati) akinywa maji ya Mradi wa Kijiji cha Shilima wakati wa sherehe za kupokea mradi huo.

# KERO ILIYODUMU KWA MIAKA SITA YAWA HISTORIA

Wananchi wa Kijiji cha Shilima, Kata ya Kikubiji Wilaya ya Kwimba, Mkoani Mwanza wameipongeza Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) kwa kukamilisha mradi wa maji uliyokuwa umesimama kwa miaka sita

Mbunge wa Jimbo la Kwimba Mhe. Shanif Mansoor (CCM) ametoa pongezi hizo kwa niaba ya wananchi hao Septemba 22, 2019 alipojumuika nao kusherehekea kukamilika kwa mradi huo ambao ulipaswa kukamilika tangu mwaka 2013 lakini kutokana na udhaifu wa Mkandarasi haukuweza kukamilika kwa wakati.

Alisema Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli ni ya vitendo, ikiahidi inatimiza kwani ameshuhudia miradi mingi ikitekelezwa kwa ufanisi na kwa wakati.

Mhe. Mansoor alisema kukamilika kwa mradi huo ni kama ndoto ambayo wananchi wake wamekuwa hawana uhakika wa lini itatokea hasa ikizingatiwa kwamba kero ya maji kwa wananchi wa Kijiji cha Shilima, Kata ya Kikubiji ilikuwa ni kubwa.

Akizungumzia historia ya mradi huo, Mhe. Mansoor alisema ulianza kutekelezwa mwaka 2013 lakini Mkandarasi alikua akisuasua na baada ya Waziri kufika kwenye eneo hilo alifanikisha kuvunja mkataba na kazi ya ujenzi wa mradi huo kukabidhiwa rasmi kwa MWAUWASA. "Namshukuru sana Profesa Mbarawa, alifika hapa na kujionea hali halisi na hatimaye alifanikiwa kusitisha mkataba na Mkandarasi na kukabidhi rasmi ujenzi wa mradi kwa MWAUWASA," alisema.

Mhe. Mansoor alitoa shukrani zake kwa Serikali kwa niaba ya wananchi wa Shilima ambapo alielezea adha waliyokuwa wakiipata kabla ya kukamilika kwa mradi huo, alisema shughuli nyingi za kimaendeleo zilisuasua kutokana na kukosekana huduma ya maji ya uhakika kwani wananchi walitumia muda mwingi kufuata maji umbali mrefu na hivyo kushindwa kushiriki kikamilifu shughuli nyingine za maendeleo.

"Kwa niaba ya wananchi wa Shilima naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano, Waziri Mkuu alifika hapa na baadaye Waziri wa maji, waliahidi na wametimiza," alisema Mhe. Mansoor.

Kwa upande mwingine Mhe. Mansoor alipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) chini ya aliyekuwa Mkurugenzi wake, Mhandisi Anthony Sanga ambaye sasa ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa kukamilisha mradi huo kwa wakati kama ilivyokuwa imeagizwa na Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa.

"Kwakweli MWAUWASA inafanya kazi kubwa na nzuri sana, kwa kipekee nampongeza sana Mhandisi Sanga kwa kuusimamia mradi huu kwa weledi mkubwa na sasa umekamilika," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Kikubiji, Alfred Luteja aliipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Wizara ya Maji ambayo ilielekeza mradi huo ukamilishwe na MWAUWASA. "Serikali yetu ni sikivu, tumeieleza na imesikia na imefanyia kazi kilio chetu, hatimaye sasa tunatumia maji kutoka Ziwa Victoria," alisema Luteja. Sherehe hizo za kupongeza mradi vilevile zilihudhuriwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Meck Manyama, viongozi mbalimbali na wananchi wa vijiji vya jirani.

Mradi wa Shilima ulizinduliwa rasmi na Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa Septemba 14, 2019 ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Maji pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inayoelekeza kuwapatia huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 85 wakazi wote waishio vijijini ifikapo mwaka 2020.

Kijiji cha Shilima ni moja ya Vijiji 12 vilivyopo kwenye utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa Mazingira Vijijini Wilayani Kwimba. Katika utekelezaji wa program hiyo, tayari vijiji vya Ishingisha, Mwabilanda, Nyambiti, Milyungu, Nyanhinga, Hungumalwa, Igunghya na Igumangobo vimeanza kutoa huduma ya maji na kusimamiwa na wananchi kupitia kamati zao za maji.

Kijiji cha Shilima kilichopo kwenye Kata ya Kikubiji kina wakazi wapatao 7,526 ambapo mradi huu wenye magati 35 una uwezo wa kuhudumia wakazi 8,750 ikiwa ni wastani wa watu 250 kwa kila gati.



Wananchi wa Shilima wakijipatia huduma ya maji kutoka kwenye mradi uliyozinduliwa hivi karibuni ambao unatoa maji kutoka Ziwa Victoria.

TUNATEKELEZA KWA VITENDO

# ZIARA YA WAZIRI MBARAWA KWENYE MRADI WA MAJI MSALALA

Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa alifanya ziara kwenye mradi wa maji wa pamoja unaohusisha Halmashauri Tatu za Msalala, Nyang'hwale na Shinyanga Vijijini maarufu kama Joint Water Partnership Project (JWPP) kwa lengo la kujionea hatua iliyofikiwa ya utekelezwaji wake.

Mradi huo utanufaisha zaidi ya wananchi 100,000 kutoka vijiji 14 ambavyo ni Mhando, Mwenge (Halmashauri ya Shinyanga vijijini), Nyugwa, Mwamakiliga, Izunya, Karumwa, Kafita, Lushimba (Nyang'hwale) na Kakola Namba 9, Rwabakanga, Busindi, Bugarama, Bushing'we, Ilogi (Msalala).

Katika ziara hiyo, Waziri Mbarawa aliambatana na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamkala ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga ambao ndio wasimamizi wa mradi kwa niaba ya Wizara ya Maji.







Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa (kushoto) akisikiliza maelezo ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Msalala kutoka kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (katikati).

# SERIKALI YAONGEZA FURAHA KWA WANANCHI KWIMBA

Mara baada ya kukamilika kwa mradi wa maji wa Shilima, MWAUWASA Bulletin, ilizungumza na wanufaika ambao walieleza hali ilivyokuwa na namna ambavyo wameupokea mradi huku pongezi nyingi zikitolewa kwa Serikali kupitia MWAUWASA.

## ALFRED LUTEJA, DIWANI KATA YA KIKUBIJI

Tangu tunazaliwa hatukuwahi kuwa na maji safi na salama katika kijiji chetu tulikuwa tukitumia maji ya kwenye mito na mabwawa hadi mwaka 2014 tulipoletewa visima saba vya hesawa katika vijiji vinne ambavyo ni Ikubiji, Mwabayanda, Mwalubunzwe na Shilima ndiyo vikawa mkombozi wetu lakini navyo havikudumu sana baadhi viliharibika na vingine havitoi maji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi hasa wakati wa kiangazi hadi sasa vimebaki viwili tu.

Tungepata maji tangu Desemba 2017 lakini mkandarasi aliyepewa kazi hiyo naye akawa kikwazo kikubwa tunashukuru maamuzi ya Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa na Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa kwa kuamua kufuta mkataba na mkandarasi huyo na kuwapa kazi MWAUWASA ambao wameutekeleza kwa miezi miwili tu.

## ANGELINA LUGEMBE

Kukamilika kwa mradi huu ni faraja hasa kwetu sisi wanawake na wasichana maana wakati mwingine mabinti walilazimika kuacha kwenda shule ili kuwasaidia mama zao kufuata maji na walikuwa wakikutana na changamoto mbalimbali njiani ikiwemo kukimbizwa na vibaka na baadhi yao walishawishiwa na wavulana njiani na kujiingiza katika mapenzi wakiwa na umri mdogo.

## ANTONY NYANDA

Tunaishukuru sana Serikali yetu kwa kutumalizia kero hii ya maji ambayo ilitusumbua sana. Tulikuwa tunafuata maji kutoka mbali sana kwenye Kijiji cha Nyabusalu nah ii ilituchukulia muda wetu mwingi hali ambayo ilisababisha tushindwe kujikita kwenye shughuli za kimaendeleo. Kwa sasa ni kufanya kazi tu kujiletea maendeleo kwani hatusumbuki tena kutembea umbali mrefu kufuata maji



ANGELINA LUGEMBE



ALFRED LUTEJA



ANTONY NYANDA



NDUGU MTEJA UNAPOHITAJI MAUNGANISHO MAPYA YA HUDUMA YA MAJISAFI NA MAJITAKA, TAFADHALI FIKA OFISI ZA MWAUWASA ZILIZO KARIBU YAKO UPATIWE HUDUMA.
USITUMIE VISHOKA ILI KUEPUKA HASARA.

KWA MAELEZO PIGA SIMU BURE
0800110023

# KUMBUKA:

**ANKARA ZA MAJI ZA MWAUWASA ZINALIPWA KUPITIA MITANDAO YOTE YA SIMU ZA VIGANJANI, BENKI NA MAWAKALA WOTE WA BENKI NCHINI.**

**KWA MAELEZO PIGA SIMU BURE**

**0800110023**

Lipa sasa kwa njia ya

tigo pesa | T-PESA | airtel money | vodacom m-pesa | halopesa | NBC National Bank of Commerce Conveniently Everywhere | CRDB BANK The bank that listens | NMB Close to you




MWANZA URBAN WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY
MWAUWASA
'Simu yangu ni Ankara yangu ya maji"
1
PIGA
*152*00#
2
CHAGUA
6. MAJI
3
CHAGUA NAMBA 4
MWAUWASA
4
CHAGUA NO. 1
DENI LA MAJI
5
INGIZA AKAUNTI
NAMBA YA MAJI
Lipa sasa kwa njia ya
tigo pesa
PESA
airtel money
vodacom
m-pesa
halopesa
NBC
National Bank of Commerce
Conveniently Everywhere.
CRDB BANK
The bank that listens
NMB
Close to you


MWANZA URBAN WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY
MWAUWASA
0800110023
Tupigie tukuhudumie
Tupigie utupe taarifa za uvujaji
Tupigie endapo kuna jambo linakutatiza juu ya huduma zetu.
TUPO HAPA KUKUHUDUMIA, TUNAKUJALI, TUNAKUBORESHEA HUDUMA
KWA MAELEZO PIGA SIMU BURE
0800110023
Mwauwasa
Mwauwasatz



# ZINGATIO LA SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA NA.5 YA MWAKA 2019

**Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Kifungu cha 61 kinabainisha "Kosa la kuharibu miundombinu ya Maji, adhabu yake ni faini ya Tsh. 5,000,000 (Milioni Tano) hadi Tsh. 15,000,000 (Milioni Kumi na Tano) au Kifungo kati ya Miaka Miwili hadi Mitano au vyote kwa pamoja."**

**Kifungu cha 62 kinaeleza "Kosa la kuiba Maji, adhabu yake ni Faini ya Tsh. 500,000 (Laki Tano) hadi Tsh.15,000,000 (Milioni Kumi na Tano) au kifungo kati ya Miezi 12 hadi Miaka Mitano au vyote kwa pamoja."**

**Kifungu cha 64 kinaeleza "Kosa la kuchezea Dira ya Maji ili kufanya udanganyifu wa Huduma ya Maji, adhabu yake ni Faini ya kuanzia Tsh. 500,000 (Laki Tano) hadi Tsh. 10,000,000 (Milioni Kumi) au kifungo cha Miezi Sita hadi Miaka Miwili au vyote kwa pamoja."**

Mwauwasa    Mwauwasatz    0800110023

# WATUMISHI MWAUWASA WAPEWA SOMO



**Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi MWAUWASA, Edith Mudogo (aliyesimama) akizungumza na watumishi wa MWAUWASA (hawapo pichani). Kushoto ni aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji, Mhandisi Anthony Sanga. Kutoka kulia ni Meneja Utawala na Rasilimali Watu wa MWAUWASA, Deogratias Magayane, Wajumbe wa Bodi, Denisa Pagula na Ellen Bogohe**

Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) wametakiwa kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yao na kufanya kazi kwa uadilifu.

Wito huo ulitolewa na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA ambaye sasa ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga wakati wa mkutano na wafanyakazi wote uliofanyikia kwenye ukumbi wa Mikutano wa Mamlaka kwenye jengo la Maji House ikiwa ni utaratibu aliyokuwa amejiwekea wa kuzungumza na watumishi wote kila mwezi.

Mhandisi Sanga alisema ili kupata matokeo chanya, watumishi wote hawana budi kuhakikisha wanafanya kazi kwa uadilifu na wanakuwa kitu kimoja na kwamba kila mtumishi anapaswa kutambua na kuheshimu nafasi ya mwenzake kwenye utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

"Hakuna mtumishi aliyebora kumzidi mwenzake, sote tunahitajiana ili kutimiza majukumu yetu na ndiyo maana kukawa na mgawanyo wa majukumu. Yatupasa tufanye kazi kwa pamoja kwa kuzingatia umuhimu wa kila mmoja wetu," alisema Mhandisi Sanga.

Mhandisi Sanga aliwakumbusha watumishi hao jukumu lao kuu ambalo ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji na aliwataka kuhakikisha wanatekeleza jukumu hilo kwa ufanisi na ubunifu mkubwa ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Alibainisha kwamba endapo kila mtumishi atatimiza majukumu yake kama inavyostahili, huduma itaboreka zaidi na maeneo mengi yatafikiwa hasa ikizingatiwa kwamba Jiji la Mwanza linakuwa kwa kasi.

"Tunapaswa kwenda na kasi ya ukuaji wa Jiji letu, hatupaswi kuachwa nyuma; kadri Jiji linavyozidi kutanuka nasi hatuna budi kutanua huduma zetu na busara zaidi ni kufika mbali zaidi kwa maana yakufika kwenye maeneo ambayo bado Jiji halijafika," alisema Mhandisi Sanga.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Edith Mudogo aliwaasa watumishi wote kuwa wazalendo na aliwataka watumie nafasi walizonazo kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji kama inavyostahili.

Alisema MWAUWASA inawatumishi wa kada mbalimbali na kwamba yampasa kila mtumishi kwa kada yake afikirie namna bora ya kuhakikisha huduma ya maji inaimarika na kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan wale wa maeneo ya pembezoni.

"Hapa tuna watumishi wa kada mbalimbali, sasa itapendeza kila mtumishi kwa kada yake atazame ni vipi anaweza kuwa na mchango wa kusambaza huduma hii ya maji kwa wananchi waishio maeneo ya pembezoni," alisema Mudogo.

Aliwahakikishia ushirikiano kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi hasa ikizingatiwa kwamba dhamira ya Bodi ni kuona wananchi wengi zaidi wanapata huduma ya maji bila kujali maeneo waliyopo.

"Sisi kama Bodi matamanio yetu ni kuona wananchi wote wa Jiji la Mwanza wanapata huduma ya maji kutoka MWAUWASA; hatupo tayari kuona mnashindwa kutimiza majukumu yenu, tupo nanyi, tufanye kazi," alisisitiza.

Aidha, mkutano huo ulitumika kutambua jitihada za watumishi waliofanya kazi MWAUWASA kwa miaka 15 ambapo watumishi sita walikabidhiwa tuzo za utumishi wa muda mrefu ikiwa ni ishara ya kutambua jitihada zao za muda mrefu katika kuwahudumia wananchi.

Tuzo hizo za utumishi wa muda mrefu hutolewa kila mwaka ambapo mtumishi anayetimiza miaka 15 hukabidhiwa ikiwa ni ishara ya kutambua utumishi wake kwa muda wote huo.



**Baadhi ya watumishi wa MWAUWASA wakimsikiliza liyekuwa Mkurugenzi Mtendaji, Mhandisi Anthony Sanga (hayupo pichani) wakati wa mkutano wa watumishi wote uliofanyikia kwenye ukumbi wa mikutano wa mamlaka maarufu kama Maji House**



**Baadhi ya watumishi wa MWAUWASA wakimsikiliza Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi MWAUWASA, Edith Mudogo (hayupo pichani) wakati wa mkutano.**

MWAUWASA
Mwanza Urban Water Supply And Sanitation Authority
NEWS BULLETIN
Oktoba 2019

# WAKANDARASI MRADI WA MAJI SAME-MWANGA WATAKIWA KUONGEZA KASI



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (wa pili kushoto) akitembelea kituo cha tiba ya maji cha mradi wa Same-Mwanga kinachojengwa na Kampuni ya M.A Kharafi & Sons.

Wakandarasi wanaotekeleza mradi wa maji wa Same-Mwanga wametakiwa kuongeza kasi ya utekelezaji wake ili ukamilike kwa wakati.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga ametoa maelekezo hayo Septemba 28, 2019 wakati wa ziara yake iliyolenga kukagua hatua ya ujenzi iliyofikiwa na Wakandarasi wanaotekeleza mradi huo ambao ni kampuni ya M.A Kharafi & Sons na kampuni ya Badr East Africa Enterprises.

Mara baada ya kujionea shughuli zilizokuwa zikiendelea na kupokea taarifa ya mradi kutoka kwa wakandarasi hao, Mhandisi Sanga alieleza kutoridhishwa na kasi ya utekelezwaji wake na aliwasisitiza kuhakikisha kuwa mradi unakamilika kwa wakati.

Mhandisi Sanga aliwataka Wakandarasi kuwa wepesi kwenye kufanya mawasiliano na Wizara kila wanapokutana na changamoto yoyote ambayo ipo nje ya uwezo wao ili ufumbuzi upatikane haraka bila kuchelewesha shughuli za ujenzi wa mradi.

"Sijaridhishwa na kasi yenu ya ujenzi wa mradi. Kama kuna changamoto mnakutana nazo zilizo nje ya uwezo wenu mhakikishe mnawasiliana na Wizara mapema iwezekanavyo ili tupate ufumbuzi," alisema Mhandisi Sanga.

Aliongeza kwamba Serikali inachohitaji ni kuona matokeo na haipo tayari kumvumilia mkandarasi ambaye anachelewesha mradi bila ya kuwa na sababu za msingi.

"Wanachohitaji wananchi ni maji, Serikali haitomvumilia Mkandarasi ambaye atashindwa kwenda na kasi inayokubalika," alibainisha Mhandisi Sanga.

Mhandisi Sanga vilevile aliwakumbusha wakandarasi hao kuhakikisha manunuzi ya vifaa vinavyohitajika kwenye ujenzi wa mradi huo yanafanyika hapa nchini badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi hasa ikizingatiwa kwamba vingi vinapatikana hapa hapa Nchini.

**INAENDELEA UK 16**



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (katikati) akitembelea kituo cha tiba ya maji cha mradi wa Same-Mwanga kinachojengwa na Kampuni ya M.A Kharafi & Sons.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (mbele) akikagua ujenzi wa kituo cha kusukuma maji (booster station) cha mradi wa Same-Mwanga kinachojengwa na Kampuni ya Badr East Africa Enterprises.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (wa tatu kutoka kulia) alipotembelea eneo la chanzo cha maji (Bwawa la Nyumba ya Mungu) cha mradi wa Same- Mwanga akimsikiliza Mratibu wa Mradi kutoka Wizara ya Maji, Mhandisi Emma Magembe.

# WAKANDARASI MRADI WA MAJI SAME-MWANGA WATAKIWA KUONGEZA KASI

**INATOKA UK 16**

Wakandarasi hao kwa nyakati tofauti walimuahidi Naibu Katibu Mkuu Sanga kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi sambamba na kuzingatia maelekezo aliyoyatoa.

Akiwasilisha taarifa ya mradi, Mratibu wa Mradi kutoka Wizara ya Maji, Mhandisi Emma Magembe alisema mradi umesanifiwa kuzalisha kiasi cha lita milioni 103.68 kwa siku ambayo ni zaidi na mahitaji yaliyopo kwa sasa ya lita milioni 78.38 kwa kutumia maji kutoka kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu na utanufaisha jumla ya wananchi wapatao 438,931 kutoka Wilaya za Same, Mwanga na baadaye Korogwe.

Mhandisi Magembe alisema mradi unatekelezwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ikihusisha ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji maji na usambazaji kwenye Mji wa Same na Mwanga na huku awamu ya pili ikihusisha usambazaji wa maji kwenye vijiji 29 vya Wilaya za Mwanga, Same na Korogwe vilivyopo kwenye eneo la mradi.

Mradi wa Same-Mwanga ni miongoni mwa miradi mikubwa inayotekelezwa na Serikali kwa lengo la kuondoa kero ya maji kwa wakazi wa Miji ya Same na Mwanga, Mkoani Kilimanjaro na baadaye Korogwe Mkoani Tanga.

Ziara hiyo ya Naibu Katibu Mkuu Sanga kwenye mradi huo ni ya kwanza tangu ameteuliwa na kuapishwa kushika wadhifa huo Septemba 22, 2019



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (kushoto) akimsikiliza Mtaalam Mshauri kutoka Kampuni ya ECG anayesimamia ujenzi wa chanzo cha maji na kituo cha tiba ya maji Mhandisi Nabil Fathy.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (wa pili kushoto) akikagua moja ya tenki la maji la mradi wa Same-Mwanga linalojengwa na Kampuni ya Badr East Africa Enterprises.



Washirika wa maendeleo wakiwa katika picha ya pamoja na watendaji Serikalini. Katikati waliokaa ni aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Emmanuel Kalobelo; kulia kwake ni Ofisa Mradi kutoka AFD, Katell Rivolet na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Jijini Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga na kushoto kwake ni Mkuu wa Msafara wa AFD, Claire Fargeaudou na Mratibu mradi kutoka EIB, Raoul Pedrazzani.

# WASHIRIKA WA MAENDELEO WAIPONGEZA MWAUWASA

Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) zimeipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) kwa umakini wake kwenye usimamizi wa miradi inayotekelezwa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ijulikanayo kama LV WATSAN.

Pongezi hizo zilitolewa na wawakilishi wa washirika hao wa maendeleo wakati wa ziara yao kwenye mradi wa maji wa Lamadi ambao ni moja ya miradi inayotekelezwa kupitia programu hiyo ya LV WATSAN.

Mratibu mradi kutoka EIB, Raoul Pedrazzani alisema miradi inayotekelezwa chini ya Programu ya LV WATSAN imeonyesha mafanikio makubwa na kwamba MWAUWASA inastahili pongezi kwa jukumu hilo la kuisimamia miradi iliyopo kwenye programu hiyo kwa umakini na weledi mkubwa kwa niaba ya Wizara ya Maji.

Pedrazzani alibainisha kwamba EIB ina nia ya dhati ya kupanua ushirikiano na Serikali ya Tanzania katika siku zijazo kwani imeridhishwa na namna ambavyo Serikali inatekeleza miradi maeneo mbalimbali kote nchini.

Naye aliyekuwa Afisa Miradi kutoka AFD, Clement Kivegalo akizungumza kwa niaba ya ujumbe alioambatana nao, alisema wameridhishwa na hatua ya utekelezaji wa mradi na kwamba AFD itaongeza udhamini kadri itakavyohitajika kufanya hivyo.

INAENDELEA UK 18



Ujumbe wa washirika wa maendeleo wakiwa katika picha ya pamoja na Watendaji kutoka Serikali kwenye eneo la chanzo cha maji cha maji mradi wa Lamadi.

# WASHIRIKA WA MAENDELEO WAIPONGEZA MWAUWASA

INATOKA UK 18

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Busega, Tano Mwera ambaye alikuwa mwenyeji wa ugeni huo wilayani hapo, alisema mradi unatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa kwenye wilaya na hususan katika mji wa Lamadi na alitoa wito kwa wawekezaji kujitokeza kwani maji ya uhakika yamepatikana na kwamba miundombinu mingine ipo vizuri ikiwemo barabara na umeme wa uhakika.

Kwa upande wake aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga akiuelezea mradi alisema unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia mia moja kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka EIB na AFD kwa gharama ya Shilingi Bilioni 12.83.

Mhandisi Sanga alisema mradi utazalisha lita Milioni 3.3 za maji kwa siku ambayo ni mara mbili ya mahitaji ya sasa ya wananchi wa Lamadi na maeneo jirani hasa ikizingatiwa kwamba mradi umebuniwa kuhudumia wananchi zaidi ya 60,000. Aliongeza kuwa hatua ya kwanza ya maunganisho kwa wananchi; mradi utaunganisha kaya zipatazo 5000 na aliwataka wananchi kuchangamkia mradi ili kujiletea maendeleo.

Kabla ya ziara hiyo, washirika hao wa maendeleo walifanya mkutano Jijini Mwanza na watendaji kutoka Serikalini kwa ajili ya majadiliano na tathmni ya hatua za zilizofikiwa kwenye ujenzi wa miradi ya maji inayotekelezwa chini ya Program ya LV WATSAN.



Washiriki wa mkutano wakikagua miundombinu ya tiba ya maji kwenye mradi wa Maji wa Lamadi. Wa kwanza ni Mratibu mradi wa LV WATSAN kutoka EIB, Raoul Pedrazzani.



Ujumbe wa washirika wa maendeleo ulitembelea maeneo mbalimbali ya mradi. Pichani ni sehemu ya eneo la Tiba ya Maji.



Muonekano wa baadhi ya maeneo ya mradi wa maji wa Lamadi ambao ulitembelewa na ujumbe wa washirika wa maendeleo.

